

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA**  
**MITAA**  
**HALMASHAURIYA WILAYA MOROGORO.**



16/03/2021

**TANGAZO LA KAZI YA UJENZI WA MAJENGO YA WODI ZA**  
**HOSPITALI YA WILAYA YA MOROGORO.**

Halmashauri ya wilaya ya morogoro imepokea fedha kutoka serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa wodi za wagonjwa za hospitali ya Wilaya ya Morogoro, hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro inawatangazia mafundi (**local fundi**) au kikundi chenye nia na uwezo wa kufanya kazi ya ujenzi kama ifuatavyo.

NA	JINA LA JENGO	NAMBA YA ZABUNI
1	JENGO LA WODI YA WATOTO (PAEDIATRIC WARD)	LGA.080/NC/PW-DH/2020/2021/01
2	JENGO LA WODI YA WANAWAKE (FEMALE WARD)	LGA.080/NC/FW-DH/2020/2021/01
3	JENGO LA WODI YA WANAUME (MALE WARD)	LGA.080/NC/MW-DH/2020/2021/01

**MASHARTI KWA WAOMBAJI LOCAL FUNDI WOTE.**

1. Mwombaji awe na uzoefu wa kujenga majengo ya serikali kwa muda usiopungua miaka mitatu(3) kwa kuonyesha orodha ya miradi aliyowahi kufanya au anayoendelea kufanya. Waombaji watatakiwa kujaza vitabu vya maelekezo na gharama (Schedule of labour) ambavyo vinapatikana ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji-Kitengo cha Manunuzi kuanzia saa 2.00 asubuhi mpaka saa 9.30 alasili.

2. Mwombaji awe na mafundi wasaidizi wasiopungua kumi (10) ili kuharakisha kazi za ujenzi.
3. Madiwani na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro hawaruhusiwi kuomba kazi hii.
4. Mwombaji aandike barua ya maombi ya kazi ya ujenzi wa jengo analohitaji, aiweke kwenye bahasha ikiambatana na nyaraka muhimu za kiufundi.
5. Maombi yote yaletwe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji moja kwa moja kwa mkono ili kuepuka kuchelewa kwa maombi au kufika baada ya siku ya mwisho.
6. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 23/03/2021 saa **nne asubuhi** ikifuatiwa na ufunguzi utakaofanyika siku hiyo katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro. (Aidha maombi yote yaletwe kwenye Ofisi za sasa za Halmashauri zilizoko Kijiji cha Mvuha).
7. Waombaji wanaruhusiwa kuwepo kwenye ufunguzi wa zabuni utakaofanyika baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi.
8. Maombi yote yatumwe kama ilivyoelekezwa katika namba 6 hapo juu kulingana na ombi la kila mwombaji kwenda kwa  
MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA MOROGORO,  
S.L.P 1880  
MOROGORO



REHEMA S. BWASI  
MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA MOROGORO